*Kiswahili, Juz. 88(2), 165-178*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Miti kama Elementi ya Udhibiti wa Miundomsingi ya Kijani katika Diwani Teule za Ushairi wa Kiswahili

*Mwaniki Mugwe*[1], *Rayya Timammy*[2] *na Omboga Zaja*[3]

**Ikisiri**

Makala hii inalenga kubainisha uanuwai wa miti kama miongoni mwa elementi asilia na ya msingi katika udhibiti wa miundomsingi ya kijani katika diwani teule za ushairi wa Kiswahili. Tumeteua diwani za ushairi za *Kina cha Maisha* (Mohammed, 1984), *Jicho laNdani* (Mohammed, 2002), *Msimu wa Tisa* (Mberia, 2007) na *Doa* (Mberia, 2018) kama vyanzo vya data yamsingi. Ili kutimiza lengo hili, tumetumia mbinu ya usampulishaji lengwa katika kuteua kazi zilizotoa data ambazo tumezichambua kwa kutumia njia ya maelezo. Fauka ya haya, tumeongozwa na Nadharia ya Fasihi Ikolojia ambayo kimsingi inaangazia uhusiano na mwingiliano baina ya binadamu na mazingira anamoishi(Glotfelty, 1996). Matokeo yanaonesha kuwa utunzajina uhifadhi wa miti ni miongoni mwa elementi ya miundomsingiya kijani ambayo hudhibiti na kufanikisha uendelevu wa mfumo tata na changamani wa uhaianuwai. Mathalani, kupitia miti, binadamu anapata afya njema, dawa na tiba za jadi na za kisasa na uimarikaji wa uchumi kutokana na rasilimali zinazozalishwa kutokana na miti. Vilevile, miti inatumika katika udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi, hifadhi ya baadhi ya spishi zawanyamapori kama vile mijusi na nyani.

## 1.0 Utangulizi

Miundomsingi inahusu ujumla wa vifaa vya kiteknolojia, majengo kama vile barabara pamoja na njia za mawasiliano zinazounda muundo wa nje wa mji. Kwa upande mwingine, miundomisingi kijani ni njia ya kubuni au kujenga miundombinu kwa kuzingatia sifa za kijani au mazingira. Kauli hii inaoana na kauli ya Hurley (2018) anayeeleza kwambamiundomisingi ya kijani hutumika kupunguza athari hasi kwa mazingira kwa kuboresha maji na hewa. Aidha, miundomsingi ya kijani inaweza kujumuisha kujenga majengo ya kijani, kutumia nishati mbadala, udhibiti wa taka kwa njia endelevu na pia kupanda miti. Katika makala hii, tumeangaziamatumizi

[1] Mwalimu wa Kiswahili, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
Baruapepe: johnmwaniki85@gmail.com

[2] Profesa, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
Barua pepe: rayya@uonbi.ac.ke

[3] Profesa mshiriki, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
Baruapepe: Ombogazaja@yahoo.com

anuwai ya miti kama mojawapo tu ya kipengele kinachounda miundomisingi kijani. Utafiti huu umechochewa na uhalisia kwamba katika karne ya ishirini na moja, ukataji na uharibifu wa miti kwa jumla umesababisha kuongezeka kwa viwango vya joto ulimwenguni na viwango vya maji katika bahari za ulimwengu (Goudie, 2019). Kulingana na kauli na madai ya Eliss(2015), mabadiliko ya tabianchi yanatokana na ongezeko la idadi ya binadamu katika mfumo anuwai wa ikolojia, na matokeo yake ni kwamba maeneo ya sehemu za mijini yanaendelea kukua na kupanuka kwa kiasi kikubwa ili kuweza kumuduidadi kubwa ya watu inayohitaji siyo tu makazi bali pia rasilimali za kimazingira ili iweze kujikimu.

Fauka ya hayo, Toigo (2015) anabainisha kuwa miti kama mojawapo ya elementi ya msingi katika miundomisingi ya kijani,huchangia kwa kiasi kikubwa katika uendelevu na ukuaji wa mfumo changamani na tata wa ikolojia. Mathalani, miti hutumika kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kudhibiti mabadiliko ya tabianchi kwa kufyonza gesi ya kaboni kutoka kwenye hewa, hutumika kama makazi ya spishi za wanyama na mimea, kama vyanzo vya chakula na hutoa mbao na boriti ambazo hutumika katika ujenzi, miongoni mwa matumizi mengine. Kutokana na uhalisia huu,tunakubaliana na kauli za Toigo (2015) na kuongeza kwamba miti hutekeleza wajibu muhimu katika mfumo wa uhaianuwai ilhali kutokuwapo kwa miti katika mazingira husababisha uhai wa binadamu na mimea kuwahatarini. Licha ya kwamba ukataji wa miti unaendelea kuongezeka hasa katika karne ya ishirini na moja, binadamu sharti ahakikishe kuwa kuna usawa wa mfumo wa ikolojia ili kuweza kuendelea na maisha yake na maisha ya spishi zingine. Masuala haya japo yameangaziwa kwa mtazamo wa kisayansi, yamepenyeza na kujumuishwa katika mawasilisho ya tungo bunilizi na za ushairi za kifasihi kama zinavyoakisika katika tungo za Mohamed na Mberia.

## 2.0 Tatizo la Utafiti

Kuna baadhi ya kazi za hivi karibuni zinazochanganua ikolojia kama suala ibuka katika fasihi ya Kiswahili. Mathalani, Sekile (2023) anazungumzia kuhusu nafasi ya fasihi mazingira katika kueleza uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Sekile anaangazia jinsi nyimbo za Mrisho Mpoto na Beka Flavour zinavyoendeleza masuala ya kiuchumi. Katika uchunguzi wake,Sekile(2023) anabainisha kwamba nyimbo ni nyenzo mwafaka katika kuelimisha jamii kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira hasa zinapoimbwa zisifu kuwapo kwa mazingira ya asili au kukashifu uharibifu wa mazingira ya asili kama vile miti na mito. Kwa upande mwingine, Muteti (2024) anazungumzia kuhusu uhusianona mwingiliano uliopo baina ya mazingira na uchumi. Anabainisha kwamba mazingira ya asili yanachangia kwa kiwango kikubwa katika kuendeleza nyenzo za kiuchumi. Licha ya kwamba tafiti hizi zinahusisha mazingira ya asili na masuala ya kiuchumi, mazingira ya asili kama vile miti yana nafasi nyingine kama vile kuendeleza uwepo wa hali njema ya kiafya na kama chanzo cha matibabu ya asili, masuala ambayo tumeyabainisha katika makala hii.

## 3.0 Nadharia ya Fasihi Ikolojia

Nadharia ya Fasihi Ikolojia kama mkabala wa kusoma, kuchanganua na kuhakiki fasihi;iliibuka katika miaka ya 1970 nchini Marekani, kisha ikasambaa huko Uingereza na hatimaye katika mataifa mengine (Glotfelty, 1996). Hata hivyo, nadharia hii iliwekewa mihimili ya kitaaluma mwaka 1996 namwanafasihi wa Kimarekeni CheryllGlotfelty.Mwanafasihi huyu anabainisha kuwa Nadharia ya Fasihi Ikolojia hutumika kuchunguza mahusiano na maingiliano kati ya kazi bunilizi za fasihi na mazingira ya asili. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa Nadharia ya Fasihi Ikolojia hujifunga tu katika uchanganuzi wa mahusiano ya fasihi, utamaduni na mazingira, bali hujumuisha na kutumika pia katika uchunguzi wa taaluma nyingine kama vile sayansi, siasa, falsafa, uchumi na kadhalika.

Changamoto ambazo huyakumba mazingira mara nyingi huhusishwana maendeleo ya kisayansi yasiyodhibitiwa kwa umakini. Hii ina maana kwamba, mijadala mingi kuhusu mabadiliko hasi ya tabianchi inahusishwa na wataalamu wa kisayansi. Hata hivyo,kulingana na kauli na hoja za Glotfelty (1996),masuala ya mazingira yanayoikumba jamii yanaweza kuangaliwa kupitia fasihi.Kutokana na kauli hii, fasihi inahusiana na kuakisi utamaduni na mazingira inamobuniwa, kauli ambayo inabainika katika tungo za ushairi za Mohamed na Mberia.Nadharia hii iliibukakama mkakati uliopania kubaini, kuelewa na kuchanganua kwa kina masuala ya kisasa ya kimazingira yanayoathiri ulimwengu kwa njia hasi. Kauli hiyo inaelekea pia kudai kwamba, kwa sasa nadharia hii imeweza kujisimamia kama mkakatiunaoeleza namna binadamu anavyohusiana na mazingira ya asili na mazingira jengwa katika tungo za kifasihi.

Mojawapo ya mihimili ya Nadharia ya Fasihi Ikolojia ni kuchunguza namna ambavyo masuala ya ikolojia, utamaduni unaohusu mazingira na mitazamo tofauti kuhusu mazingira inavyosawiriwa katika kazi za kifasihi. Mhimili huu umetuwezesha kubainisha jinsi mazingira kama zao la kitamaduni yanavyotumika kwa mfano kama chanzo cha dawa na matibabu. Aidha, nadharia hii hutumika kusisitiza uwepo na umuhimu wa binadamu na spishi zingine za wanyama na mimea katika mchakato mzima wa uhaianuwai. Mhimili huu umetuwezesha kuangazia miti kama mojawapo ya elementi muhimu ya miundomsingi kijani inavyotumika kuboresha uhai wa binadamu na viumbe vingine. Mathalani, katika muktadha huumiundomisingi kijani hujumuisha miti ambayo hujitokeza katika miktadha ya kiasili na miktadha jengwa na pia ni mojawapo ya spishi za mimea zinazopatikana katika mfumo changamano na tata wa ikolojia.

## 4.0 Miti kama Elementi ya Udhibiti wa Miundomisingi ya Kijani katika Ushairi wa Mohamed na Mberia

Miti ni uhalisia wa kiikolojia ambao binadamu anaingiliana nao kwa kiasi kikubwa katika kila kipengele chake cha maisha. Kwa mujibu wa kauli na madai ya Jessic, Skoff na Cavender (2019), miti ina majukumu na manufaa mengi, yaliyo ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja katika mfumo wa uhaianuwai.Kutokana na

manufaa haya ya kijumla ya miti, pasina shaka, binadamu ana jukumu na wajibu wa kuhifadhi na kutunza mazingira. Japo kauli kama hizi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira zinajitokeza katika nyanja za kisayansi, pia zinajitokeza katika mashairi ya Mohamed na Mberia, kutokana na uhalisia kwamba kuna ukuruba wa karibu kati ya sayansi na kazi za kisanaa kama anavyodai Buell (2005). Mfano mwafaka wa kuthibitisha kauli kama hii unapatikana katika diwani ya *Kinacha Maisha* katika shairi "Ganga Shina" lifuatalo:

*Makongwe yanayokera yakate kwa maumivu*
*Na mizizi ya safura iliyo mikandamivu*
*Usiwe nayo subira katika utimilivu*
*Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki*

*Rasharasha sio bora dawa iwe rovurovu*
*Imwaile imara hadi isombe kitovu*
*Uchome moto sangara mti uwe muangavu*
*Ganga shina la uhai tanzuze hazigangika*

*Fyekafyeka mipapura mimea mitatagivu*
*Inayonyonya ujira wa miti mishughulivu*
*Nasaha zangu dharura kesho utakula mbivua*
*Ganga shina la uhai tanzuze hazigangika*

(Mohamed, 1984:9)

Katika beti hizi, mtunzi amesawiri miti kwa kudokeza tu kwamba miti ni sehemu ya msingi ya ikolojia ambayo humnufaisha binadamu kwa mengi katika maisha yake. Usawiri huu unasawiana na mawazo ya kisayansi na kiikolojia yanayohimiza binadamu kupanda na kuitunza miti. Kwa kuwa, mbali na kuwa miti ni sehemu ya miundomsingi ya kiikolojia, miti inatekeleza majukumu mengi pia ambayo, japo kimsingi yanahusiana na dhana nzima ya kuhimili maisha, yanaashiria pia utegemeano na uathiriano ulioko kati ya binadamu, wanyama, uhaianuwai na miti (Garibaldi, 2013). Kwa hivyo, katika usemi mfupi sana kama huu '*ganga shina'* mtunzi anawasilisha falsafa nzima inayohimili haja ya upanzi, utunzaji na uhifadhi wa miti. Katika mshororo wa kwanza usemao:'Makongwe yanayokera yakate kwa maumivu' ambao ni wito wa kufyeka na kuondoa miti mikongwe ili kuipa miti mipya fursa ya kuchipua na kuanza mduara mwingine wa maisha kujiridhisha kama miti na kuwaridhisha binadamu na viumbe wote wanaotegemea miti. Katika mshororo wa pili:'Na mizizi ya safura iliyo mikandamivu' mtunzi anarejelea hali ya mizizi ambayo inaathiriwa na ugonjwa wa safura kiasi kwamba mikinda au miche ya miti michanga imekufa, 'mikindamivu'. Binadamu anawajibishwa kuitunza na kuilinda miti, hii ndio maana katika mshororo wa tatu, mtunzi anahimiza:'Usiwe nayo subira katika utimilivu', yaani binadamu asifanye ajizi na uzohali wa kukawia kutekeleza wajibu wake kwa miti. Mtunzi anahimiza kuwa kuwajibika huku kunahusu kuondoa maganda makongwe yaliyo kwenye miti, kuondoa mizizi

iliyoathiriwa na ugonjwa ambao unakandamiza shina. Kulingana na madai ya Nadharia ya Fasihi Ikolojia, ni jukumu la binadamu kutunza na kuhifadhi mazingira. Madai haya yanaakisika katika beti hizi mtunzi anaposawiri jinsi binadamu anavyotunza na kuhifadhi miti.

### 4.1 Udhibiti wa Afya na Hali Njema

Miti pia inahusishwa na afya na uwepo wa hali njema katika jamii (Jessical, Skoff na Calevender, 2019). Suala hili linatokana na uwezo wa miti kufyonza vichafuzi kutoka kwenye hewa. Tafiti zinazoangazia suala hili la vichafuzi vya hewazinaonesha kuwa hewa katika sehemu ambazo hazina miti inaweza kuathirika kwa njia hasi na kuchangia uibukaji na ueneaji wa maradhi kama vile ya glakoma yanayoathiri macho na kutatiza kuona (Berhane, 2016; Zhong na wenziwe, 2016; Di, 2017). Kimsingi, miti inachuja hewa chafu na kupunguza maradhi ya upumuaji yanayoua idadi kubwa ya watu duniani (Nowak na Greenfield, 2018). Fauka ya hayo, wataalamu hao wanadai kuwa uwepo wa miti na mazingira ya kijani unahusishwa kwa kiasi kikubwa na upunguzaji wa fikra na mawazo hasi, upunguzaji wa dalili za mfadhaiko, uwepo wa hali chanya ya moyo na utoshelevu wa maisha. Kauli kama hizi zinaakisika kwenye diwani ya*Jicho la Ndani* katika shairi “Kadhia ya Miti”, Mohamed (2002: 34) anaposema:

*Zilipovuma kwa ‘pole pepo zilizo mwanana*
*Kuwapoza na vilele na walio kwenye shina*
*Na vivuli vizingile joto likashuka kina*
*Nyoyo kutazama mbele maisha yalivyofana*

Katika ubeti huu, mtunzi anatambua umuhimu na manufaa ya miti inayochangia kuwapo kwa hali tulivu inayoliwaza nyoyo za binadamu, wadudu na wanyama kwa jumla:‘Na vivuli vizingilejoto likashuka kina’. Uwepo wa kivuli na upepo mwanana unashusha kiwango cha joto kinachoweza kuathiri afya ya binadamu na viumbe wengine, na uwepo wa upepo unaboresha hali ya fikra na saikolojia ya binadamu:‘Nyoyo kutazama mbele maishayalivyofana’. Kuna masuala mengi ya kiikolojia yanayojitokeza katika ubeti huu, japo kwa njia fiche. Mathalani, utegemeano na uathiriano wa miti na kasi ya upepo, miti inavyonufaisha wategemeao mashina na wale wategemeao vilele vya miti. Aidha, uwepo wa vivuli kukinga miale hatarishi ya jua na kukidhi mahitaji ya kibiolojia ya maisha ya binadamu, ni masuala ya kiikolojia yanayozungumziwa na mwandishi na yanaakisi Nadharia ya Fasihi Ikolojia kuwa kuna uhusiano na utegemeano kati ya viumbe na spishi zingine katika mfumo ikolojia. Suala sawia na hili limewahi kuangaziwa na kujadiliwa katika tafiti za kifasihi. Mathalani, Karoli (2023) anatoa kauli kwamba miti na baadhi ya mimea kama vile matango yalitumika kama chakula ambacho kina virutubishi ikiwamo protini, madini ya chuma na kalsiamu katika jamii za Waswahili. Karoli anabainisha kwamba matango hayo yana asidi ya mafuta ya *omega 3* ambayo ni muhimu sana kwa afya ya moyo na ukuaji wa ubongo hasa kwa

watoto wachanga. Matango pia hutumika kama dawa ya kupunguza viwango vya sukari kwenye damu kwa watu wenye kisukari, kupunguza msongo wa mawazo na pia kutumiwa kama kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

**4.2 Chanzo cha Dawa na Tiba**

Miongoni mwa masuala tawala katika baadhi ya mashairi ya Mohamed na Mberia, ni usawiri wa miti katika tungo zao kwa njia mbalimbali. Miti imesawiriwa ili kusifia urembo wake unaoweza kubadilisha mandhari kwa njia nyingi.Pia, katika baadhi ya tungo miti imesawiriwa kuwa ni chanzo na kanzi kubwa ya dawa na tiba. Usawiri huu wa kiubunifu unalandana kwa njia mbalimbali na uhalisia wa tafiti za kisayansi za hivi karibuni zinazotanababhisha kuwa kuna zaidi ya spishi 50,000 za miti ambazo zimethibitishwa kuwa na manufaa kama vyanzo vya dawa na tiba za aina mbalimbali (The World Forest Organization, 2022). Kwa mujibu wa tafiti za shirika hili, binadamu amekuwa akitumia tiba zinazotokana na miti tangu jadi, suala ambalo limechangia kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha biashara ya dawa na tiba kote duniani. Dawa hutoka katika sehemu mahususi za miti kama vile: magome, maganda, mizizi, matawi, mizizi na matunda (Global Trees Campaign, 2020). Kulingana na shirika hili, miti inachukua asilimia kubwa katika biashara ya dawa duniani huku ikizingatiwa kuwa kuna aina nyingi za molekuli zinazochukuliwa kutoka kwenye miti kwa ajili ya utengenezaji wa dawa. Kutokana na kauli hizi, tunadai kuwa uziduaji endelevu wa dawa zinazotokana na miti ni shughuli inayochangia kuinua na kuimarisha thamani ya miti na afya ya binadamu. Hoja hii ni kweli wakati inapokitwa katika misingi ya sayansi, lakini kama tulivyoeleza hapo awali, tungo za kifasihi zinatambua kuwa miti ni vyanzo vya dawa. Kwa mfano, katika diwaniya *Msimu waTisa*, shairi la“Nyanda za Minga”, mtunzi anasema:

*Nasimama na moyo wa huzuni kilimani*
*Nikitazama tambarare ya minga na njaa*
*Mgonjwa anayeendelea kuteseka kitandani*
*Akiangalia kwa macho ya kutojali-hali*
*Akisubiri daktari mzembe anayesinzia jijini*

*Kwa mgonjwa maarufu aitwaye Afrika*
*Anayelala kwenye mkeka wa mikindu*
*Kandokando mwa mizizi yenye dawa*
*Akituma aitiwe mtaalam kutoka ng’ambo*
*Aje na dawa za ugonjwa wa kulemaza*

(Mberia, 2007: 52)

Katika beti hizi, mtunzi anamtahadharisha mgonjwa kuyaangalia mazingira yake, kuyaelewana kujinufaisha nayo. Mtunzi anaisawiri miti kwa ujumla, kiasi kwamba kule kutajwa kwa miti kwa ujumla au kuangazia sehemu za miti kama vile: mizizi, magome, matawi, matunda, mbegu na mauakunaashiria utumizi wa miti kama chanzo cha tiba. Katika shairi hili, mtunzi anaangalia mazingira kwa mtazamo

uliobanwa katika muktadha mahususi kuhusu bara la Afrika linalokumbwa na magonjwa mbalimbali yanayosababishwa na umaskini, uzembe, kutowajibika na ukosefu wa utaalamuwa kisasa wa kukabiliana na magonjwa haya. Hii ndio maana mtunzi analiangalia bara zima la Afrika kama mgonjwa anayehitaji kutibiwa kwa dharura anaposema:'Kwa mgonjwa maarufu aitwaye Afrika'. Huu ni usawiri wa Afrika kwa mkabala wa ujinga na kutokujua. Ingawa mtunzi ana uhuru wa kiutunzi wa kuwasilisha fikra na uelewa wake wa masuala mbalimbali, uhalisia ulioko unaweza kuthibitisha kwamba wakazi wa Afrika wanajulikana kuwa na ukuruba wa karibu na matumizi ya miti shamba. Hata hivyo, kauli ambayo mtunzi anaelekea kuiwasilisha ni kwamba, kuna ukosefu wa uelewa wa manufaa ya miti kama dawa na mbinu zalishi za kisasa za dawa kutoka kwenye mizizi ya miti na hasa ya asili. Waafrika wengi wanabaki katika hali hoi huku wakingoja wataalamu kutoka ng'ambo kuwaletea tiba na matibabu kama mshororo huu unavyodokeza:'Akituma aitiwe mtaalamkutoka ng'ambo'. Japo kwa njia fiche, mwandishi anatoa wito kwa wakazi wa Afrika kujibidiisha na kugundua umuhimu na thamani ya tiba inayofichama katika aina mbalimbali ya miti. Aidha, suala la muhimu linalochimuza katika beti hizini kwamba kuna haja ya binadamu kupanda na kuhifadhi miti ya asili ambayo inatumika katika kuzalisha dawa zinazotumika kama tiba za asili. Kauli kama hizi zinawasilishwa na Karoli (2023) anayeeleza kwamba mitishamba mingi hutumiwa na Waswahili kwa mahitaji ya dawa. Kwa mfano, miti kama vile mikilifi au miarobaini hutumika kutibu magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kisukari na shinikizo la damu.

**4.3 Rasilimali za Miti na Udhibiti wa Uchumi**

Mitiina manufaa ya kiuchumi katika kuchangia kupunguza viwango vya umaskini na hata tishio la umaskini kwa kuongeza thamani ya rasilimali, ustawi wa uchumi na hata kuwavutia watalii kama inavyoakisika katika tungo za ushairi za Mohamed na Mberia. Kwa mujibu wa kauli na madai ya Nesbitt (2017) na Turner (2020), miti hutumiwa kuondoa au kupunguza viwango vya umaskini, kuimarisha kilimo endelevu, kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya gharama nafuu ya kuaminika na ya kisasa kwa wote. Miti huchangia kupatikana kwa nafasi za ajira miongoni mwa nchi na kuhakikisha uzalishaji na ulaji endelevu. Kutokana na uelewa wa kauli hizi, tunaweza kubainisha kuwa uharibifu wa miti ni njia mojawapo ya kuangamiza maisha ya wanajamii kwa ujumla. Kwa mfano, Turner (2015) anatoa kauli kwambamiti ikikatwa pasipo kufuata kanuni za sera zinazodhibiti ukataji huu, wanajamii ambao hutegemea mapato yanayotokana namiti wanaathirika kwa njia hasi. Kwa mfano, wanajamii wanakosa karo ya kulipia watoto wao gharama za shule na hata fedha za kuwanunulia watoto wao sare za shule na kuvuruga mzunguko duara wa uhaianuwai. Zaidi ya haya, jamii inapokosa njia za kujipatia riziki namatumizi ya kawaida, kunaibuka migogoro ya kiuchumi kati ya makabila mbalimbali. Suala la msingi la kiikolojia linalojitokeza hapa ni kwamba, kuna utegemeano wa karibu sana kati ya miti na hali ya kiuchumi; umaskini au utajiri na

upatikanaji wa chakula. Kwa usemi mwingine, miti inaathiri kila kipengele cha maishaya binadamu. Uhalisi huu unaakisika katika diwani ya *Doa* shairi la 22, mtunzi anaposema:

*Uhaba wa maji ya matumizi ya nyumbani*
*Utovu wa nywisho za mifugo na wanyama pori*
*Kukata roho ya chemchemi, mito na vijito*
*Si mchezo wa komwe kwenye ubao wa bao*
*Ni kuunda kesho ya madimbwi ya damu*
*Makabila na koo mbalimbali zikitafunana*
*Ni maandalizi ya kuingia nyua za kuzimu*

*Panga za ulafi zikiangamiza zulia la kijani*
*Ardhi ikivuliwa nguo thabiti ya maumbile*
*Ikisalia uchi ja jongoo, changara au kiboko*
*Miali ya jua ikifurahia kupiga mbizi ardhini*
*Maji kwenye udongo yatatorokea mbali*
*Udongo utakuwa bahili kwa mtama na pojo*
*Itateseka mipaipai, midimu na miparachichi*

*Kukejeli na kushambulia mazingira kwa inadi*
*Si kuuna utajiri wa kusambaza uchangamfu*
*Ni kuandaa kugongana panga za hasira*
*Si kujenga msingi wa amani na maendeleo*
*Ni kualika harufu ya matanga kwenye pua*
*Vijiji vikiwania maji ya mabwawa ya kijani*
*Baada ya mito kukata tama na kukauka*

(Mberia, 2018: 89)

Katika beti hizimtunzi anaashiria masuala mengi ya kiikolojia, yakiwamo athari hasi zinazotokana na ukataji wa miti kiholela na ukosefu wa maji nyumbani:'Uhaba wa maji ya matumizi ya nyumbani';kuharibiwa kwa vyanzo vya maji, yaani chemichemi, mito na vijito;kuwapo kwa uwezekano wa mivutano ya siku za baadaye, kung'ang'ania rasilimali asilia, uwezekano wa kutokeakwa vita na kadhalika. Kwa mtazamo mpana, mtunzi anabainisha kwamba matumizi mabaya ya rasilimali asilia ya mazingira, hayasababishi athari za kiikolojia peke yake, bali yanasababisha pia vita na migogoro kati ya jamii mbalimbali: '*Makabila na koo mbalimbali zikitafunana.'*Uhasama unaorejelewa hapa kati ya koo na makabila, ni suala linaloweza kuhusishwa moja kwa moja na athari hasi za kuharibiwa kwa mazingira asilia na hasa ukataji wa miti kiholela. Mathalani, ukaukaji wavisima vya maji, mito na vijito unatokana na athari hasi za ukataji wa miti pasipo kuzingatia taratibu na kanuni mwafaka. Uhasama huu una uwezekano mkubwa wa kusababisha vita vya kiukoo na kikabila vinavyovuruga mshikamano na utulivu wa mfumo wa ikolojia, ishara kwamba kuna uhaba wa maji katika makazi ya binadamu kutokana na uhaba wa miti.

Mjadala kama huu umewahi kujadiliwa na Sekile (2023) na Mutei (2024). Wasomi hawa wakizungumzia kuhusu mahusiano ya fasihi mazingira na nyenzo za kiuchumi, wanatoa kauli zinazosawiana kuwa katika hali halisi uchumi wa taifa unategemea sana uhai wa mazingira. Aidha, wasomi hawa wanabainisha kwamba vipengele vingi vya maisha ya mwanadamu vinategemea uhai wa mazingira. Hata hivyo, katika maisha ya kisasa wanajamii wanasaka utajiri huku wakiharibu mazingira wanamoishi.Shughuli za kiuchumi zinapaswa kusaidia kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mifumo ya kiikolojia na mahitaji ya msingi ya ustawi wa jamii imelindwa. Kwa hivyo, fasihi mazingira ina majukumu ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kwa ujumla kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

### 4.4 Miti kama Malighafi ya Uzuiaji na Udhibiti wa Mabadiliko ya Tabianchi

Miongoni mwa masuala yaliyo na mwegemeo wa kimazingira yanayojitokeza katika mashairi ya Mohamed na Mberia, ni masuala yanayohusiana na miti ambapo watunzi hawa wanasifia miti kwa kuirembesha dunia au wanaibua mijadala kuhusiana na haja ya kutunza na kuhifadhi miti kwa sababu ya manufaa anuwai yatokanayo na miti. Ujitokezaji wa masuala haya unaakisi ukweli ulioko wa kisayansi kwamba miti hutumika kwa njia mbalimbali kudhibiti mabadiliko ya tabianchi (Patz, Campbell na Hollowa, 2005).

Licha ya kwamba miti inatekeleza majukumu ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi, shinikizo la maisha ya binadamu humlazimu binadamu huyo kutaka kujikimu kiuchumi kwa kutekeleza shughuli kama vile kilimo. Hata hivyo, shughuli chanya kama za kilimo zinaweza kuwa na matokeo hasi yasiyotarajiwa kama vile kushawishi kutokea kwa baadhi ya vizingiti vinavyokwamisha juhudi za kukabiliana na tatizo hili (Ward na Lauf, 2016). Kwa mfano, wakulima wanalazimika kukata miti ilikupata nafasi ya kuanzisha mashamba au kustawisha makazi. Huu ni ukweli ambao binadamu hawezi kupuuza ingawa shughulihizi zinahitajika kufanywa kwa uadilifu na kwa makini kwa sababu utekelezaji wake kiholela mara nyingi husababisha mabadiliko ya tabianchi. Kauli sawia nahii ndiyo inayojitokeza kwenye diwani ya *Doa* katika shairi la 22, mtunzi anaposema:

*Wakulima wamechinja miti kwenye kingo*
*Samaki hawana utuvu wa kustawisha uzazi*
*Watu waliokuwa wakifaidi ukarimu wa miti*
*Leo ni mateka wa ukosefu wa lishe bora*
*Kama kwamba jua lina kiu kisichokatika*
*Ulimi wake mpana unarambaramba maji*
*Kwa mvukizo unaorindima mchana kutwa*
*Mhimili wa uhai unaotiririka mabondeni*
*Unakwapuliwa na kusambazwa angani*
*Ndivyo mito iachwayo na sura na huzuni*

*Kesho itakapobisha na kuingia nyumbani*
*Uhalisia wa mazingira utakuwa bahili*
*Usishangae kushuhudia mieleka mikali*
*Kila kundi liking'ang'ania kukidhi haja*
*Katika madimbwi yaliyosalia ya uhai*

(Mberia, 2018: 88)

Katika nukuu hii, mtunzi anasawiri jinsi ambavyo binadamu anakata miti na kuasisi shughuli za kilimo kandokando ya mito: '*Wakulima wamechinja miti kwenye kingo'*. Pamoja na kwamba binadamu anafanya haya kutokana na uwepo wa sababu halali, kitu ambacho mtunzi anataka kiangaziwe, ni utekelezaji mbaya wa shughuli hizo, yaani usiojali uendelevu wa kilimo hicho wala athari zisizokusudiwa kwa mazingira na kwa viumbe wengine wanaotegemea mazingira hayo. Ukataji wa miti, licha ya kusababisha mmomonyoko na mtelezo wa ardhi, halikadhalika unasababisha maji ya mito kukauka kwa sababu ya miale mikali ya jua kuachiwa nafasi kubwa na kusababisha kiwango kikubwa cha uvukizaji:'Kama kwamba jua lina kiu kisichokatia-Ulimiwake mpana unaramba maji'. Kuathiriwa kwa kipengele kimoja cha mazingira, aghalabu huwa na matokeo hasi kama vile kupungua kwa kiwango cha uzalishaji wa chakula na kuathirika kwa vyanzo vinavyohusiana na uzalishaji wa chakula. Pamoja na kwamba inaweza kuonekana kuwa mtunzi anawalaumu wakulima kwa kutoheshimu sheria na kanuni zinazodhibiti ukataji wa miti, hizi ni lawama zilizo na ushauri kwamba, kuna haja ya kuwa na tahadhari katika shughuli zote za matumizi ya rasilimali kama vile kukata miti pasi kujali madhara yake ya baadaye. Kauli kama hizi zinaoana na kauli za Wesonga (2021) anayeeleza kwamba miti ina majukumu faafu katika kudhibiti mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo,ni jukumu la binadamu kuhakikisha kwamba anahifadhi na kulinda miti inayomzunguka.

**4.5 Miti kama Hifadhi na Makazi ya Wadudu na Ndege**

Uwepo wa miti kama hifadhi na makazi ya wanyama ni miongoni mwa masuala anuwai yanayoakisika katika mashairi ya Mohamed na Mberia. Katika tungo zao wanadhihirisha wazi kwamba kuna mahusiano na utegemeano wa karibu kati ya miti na wanyama pori. Kauli sawia na hii inatolewa na Sereba (2016), kuwa katika mfumo duara wa uhaianuwai, miti hutumika kama makazi ya ndege, wadudu na baadhi ya spishi za wanyama. Mahusiano haya kati ya miti na wanyama yanaboresha uendelevu wa mfumo changamano na tata wa uhaianuwai. Hata hivyo, mahusiano haya yako katika njiapanda kutokana na jinsi binadamu anavyoendelea kuharibu makazi ya wanyama kutokana na ukataji wa miti kiholela. Tunaweza kutoa kauli kwamba, mahusiano kama haya kati ya miti na wanyamapori, haikosi ndio yaliyomchochea Mohamed kutunga shairi la"Kadhia ya Miti" katika diwani ya*Jicho laNdani*. Katika shairi hilo, msanii anasema:

*Mtini uliposheheni kwa utomvu wa ujana*

*Kiale hadi shinani vyema umeviringana*
*Na kijani matawini maua yakipachana*
*Ulialika wageni mtini kutulizana*

*Kaalika vipepeo wajile kuzaliana*
*Nyuki 'kaja kwa zongeo asali kuja 'ivuna*
*Hata ndege warukao maua kufyonza sana*
*Ukashamiri upeo matunda kuzaliana*

*Chungu waliposturi mtini wakipishana*
*Siafu pasi kadri wali'wakifukuzana*
*Wakitafuta sukari humo ilimojazana*
*Wakapashana habari kwa wingi kujalizana*

*Mapigi wakanisai wakapura kwa hiana*
*Na vitawi wakahasi tumbaze wakazichana*
*Zikanyongeza nafusi mti 'kukaukiana*
*Ukanawiri utesi kaumu ikagombana*

*Mijusi il'o katili kanyemelea vinona*
*Walipozusha dhilali ya vidudu kutafuna*
*Utulivu na idili ilipopoteza ma'na*
*Baini hiyo dalili ya mti haupo tena*

(Mohamed, 2002:34)

Hapa mtunzi, ametaja na kuidhihirishia jamii manufaa ya miti kama nguzo ya uhai wa viumbe ambao hatimaye humnufaisha na kumfadhili binadamu:'kaalika vipepeo wajilekuzaliana' akijua vizuri sana kwamba mbali na kuendeleza kizazi chao, vipepeo wananufaishwa na chavua ambazo pia wanazisafirisha kuwezesha kufadhili na kuendeleza maisha ya aina nyingine ya viumbe wengine. Kwenye miti, mtunzi anabainisha kwamba kuna makao, maua, chavua, matunda na hifadhi.Huu ni uchangamani sambazi wa utegemeano na uathiriano wa miti na kila aina ya maisha, na katika uathiriano huu ndipo unapowezeshwa uendelevu wa mzunguko mduara wa uhaianuwai. Kauli kama hizi zimewahi kujadiliwa katika tasnia za kiusomi. Hata hivyo, mtunzi anatoa lalamiko kuwa makazi hayo ya wadudu na ndege yanaharibiwa kutokana na matendo hasi ya binadamu ya kukata miti:'Mapigi wakarisasi wakapura kwa hiana' na 'Zikanyongeka nafusi mti'kukaukiana'. Katika nukuu hii inabainika kwamba binadamu anapura matawi ya miti na kuharibu maua ambayo yanafumba kabla ya kuchanua. Matokeo ya hali hii ni matawi ya miti kukauka na wadudu kukosa mahali pa kuishi. Hali hii inahatarisha maisha ya wadudu hawa ambao wanashambuliwa na maadui:'Mijusi wakanisasi wakapura kwa hiana', 'Walipozusha dhilali ya vidudu kutafuna'.Kulingana na mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Fasihi Ikolojia ni jukumu la binadamu kutunza na kuhifadhi mazingira yanayomzunguka. Hata hivyo, katika huu muktadha matendo ya binadamu ya

kuharibu miti ambayo ni baadhi ya makazi ya wadudu na ndege yanaenda kinyume na madai ya Nadharia ya Fasihi Ikolojia.

Mijadala na kauli mbalimbali kuhusiana na matumizi ya miti kama hifadhi ya wadudu na spishi zingine imewahi kusawiriwa na kujadiliwa katika tafiti za kifasihi. Mathalani, Sekile (2023) anabainisha na kutoa kauli kwamba ulimwengu umezungukwa na mambo mengi yanayosababisha uharibifu wa mazingira. Binadamu akiendelea kuingiliana na mazingira ya asili kwa njia hasi kama vile ukataji wa miti, anaathiri maisha ya viumbe wengine kwa njia hasi. Sekile anaibua kauli kwamba ukataji holela wa miti huharibu makazi ya baadhi ya viumbe ambao huhama katika mazingira yao ya asili na hata wengine kuangamia. Kwa hivyo, kuna haja ya binadamu kuelimishwa kuhusu manufaa ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira na hususani miti ambayo huzisitiri baadhi ya spishi katika mfumo wa uhaianuwai.

## 5.0 Hitimisho

Kupitia tungo za ushairi wa Mohamed na Mberia imebainika kwamba binadamu akiwekeza katika upanzi na uhifadhi wa miti, ataimarisha ukuaji na uendelevu wa mfumo mzunguko wa uhaianuwai. Mathalani,kwa kupitia mashairi yao, uelewa wa kina kuhusu uanuwai wa miti una manufaa mengi katika maisha ya binadamu na mazingira kwa jumla. Upanzi, utunzaji nauhifadhi wa miti, ni mojawapo ya njia mwafaka ya binadamu kuweza kukabiliana na changamoto zinazomkumba katika hali yake ya kawaida katika maisha pasi kutumia nguvu nyingi na rasilimali nyingi. Aidha, kupitia mashairi yaomiti imesawiriwa kama kigezo muhimu katika kuboresha maisha ya binadamu na huwa na mafao mengi kwa jamii. Mathalani, katika mashairi yao inabainika kwamba miti hutumika kudumisha afya na hali njema, hutumika kama chanzo cha dawa na tiba, hudhibiti mabadiliko ya tabianchi, hukuza uchumi, na hutumika kama makazi ya wadudu na ndege. Kimsingi, uakisikaji wa masuala haya katika diwani teule za ushairi unaonesha ukuaji wa ushairi wa Kiswahili katika kuelezea masuala ya kiikolojia ambayo kimsingi ni masuala ya kisayansi.

## Marejeleo

Berland, A. (2017) “The Role of Trees in Urban Stormwater Management.Landscape and Urban Planning”. *Environmental Design Research Association*, Juz.162 (1): 167-177.

Braden, B. na Johnston, D. (2004) “*Downstream Economic Benefits from Storm-water Management*”. Kongamano la 32 la Universities Council on Water Resources Lilifanyika tarehe 22 Julai 2024 South Illinois University

Buell, L. (2005) *The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Study*. Oxford: Blackwell Publishers.

Ellis, E. (2015)“Ecology in an Anthropogenic Biosphere. Ecological Monographs Journal”. *Nature Communications Journal*, Juz. 85 (3): 287-331.

Garibaldi, L. (2013) “Wild Pollinations Enhance Fruit Set of Crops Regardless of Honey Bee Abudance”. *Science Journal*, Juz. 339 (6127): 1608-1611.

Garrad, G. (2004) *Ecocriticism.* New York: Routledge Publishers.

Global Trees Campaign (2020) “Medicine Global Trees” Inapatikana katika https://globaltrees.org. Ilisomwa tarehe 12 Mei 2023.

Glotfelty, C. (1996). *Ecocriticism Reader: Landmarks* in *Literary Ecology.* Athens and London: The University of Georgia Press.

Hurley, P: na Emery, M. (2018) “Locating Provisioning Ecosystem Services in Urban Forests: Forageable Woody Species in New York City”. *Landscape and Urban Planning Journal*, Juz.170 (4): 140-149 .

Jessical, B., Skoff, T. na Cavender, N. (2019) “The Benefits of Trees for Livable Sustainable Communities”. *New Phytologist Foundation*, Juz.1 (14): 323-335.

Karoli, B. (2023) *IsimuIkolojia ya Leksimu za Miti Shamba katika Lugha ya Kiswahili*.Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Mberia, K. (2007) *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

________ (2018) *Doa*. Nairobi: Marimba Publishers Limited

Mohamed, S. A. (1984) *Kina cha Maisha.* Nairobi: Longhorn Publishers.

________ (2002) *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mutei, M. (2024)“Nafasi ya Mazingira katika Jamii kama Inavyodhihirika katika Kazi Teule za Fasihi.” *Jarida la Afrika Mahariki*, Juz.7 (2): 242-253.

Nesbitt, L; Hott, N; Barron, S; Cowan, J na Stephen, R.J. (2017) “The Social and Economics Value of Cultural Ecosystem Services Provided by Urban Forests in North America: A Review and Suggestions for Future Research”. *Urban Forestry and Urban Green*, Juz. 25 (2): 103-111.

Nowark, D.na Greenfield, E. (2018) “US Urban Forest Statistics, Values and Projections”. *Journal of Forestry,* Juz. 116 (2): 164-177.

Nowark, D; Crane, D; na Jack, S. (2006) “Air Pollution Removal by Urban Trees and Shrubs in the United States”. *Urban Forestry and Urban Greening,* Juz 4 (1):115-123.

Patz, J., Campbell, D.na Hollowa, T. (2005) “Impact of Regional Climate Change on Human Health”. *Nature Journal*, Juz. 438 (70): 310-317.

Savatree (2016) “Importance and Value of Trees”. Inapatikana katika http://www.savatree.com/whytree.html. Ilisomwa tarehe 13 Mei, 2023.

Sekile, R. (2023) “Nafasi ya Fasihi – Mazingira Kuelekea Uchumi wa Viwanda Tanzania”. *Journal of Arts and Social Sciences*, Juz.8 (2): 51-58.

Sereba, K. (2016) “Gardening for Wildlife”. Inapatikana katika https://www.rspb.org.uk. Ilisomwa tarehe 13 Mei, 2023.

Toigo, M; Vallet, M; Perot, T; Bontemps, J; Piedallu, C, na Courbaud, M . (2015) “Overyielding in Mixed Forests Decrease with Site Productivity”.*Journal of*

*Ecology*.Juz.103 (2): 502-512. DOI: http://dx.do.org/10.1111/1365/1365-2745.12353

Turner, L. (2020) “Climate Change, Ecosystems and Abrupt Change”.*Journal of Philosophical Transactions of Royal Society*, Juz.3 (7):1-2. DOI: http://dx.do.org/10.1098/rstb.2019.0105

United Nations (2015) “World Population Propespects: The 2015 Revision. United Nations Department of Economic and Social Affairs Population Division”.Inapatikana katika httsps://esa.un.org.Ilisomwa tarehe 10 Mei 2023.

Ward, K; Lauf, S.; Birgit, K; na Endlicher, W. (2016) “Heat Waves and Urban Heat Islands in Europe. A Revie of Relevant Drivers”. *Science and Environment Journal*. Juz. 569 (570): 527-539.

Wesonga, L. (2021) *Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Mazingira kupitia Riwaya Teule zaKiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Mount Kenya; Nairobi.

World Forest Organization (2022)“The Medicinal Properties of Trees”. Inapatikana katika https://www.wordforest.org. Ilisomwa tarehe 9 Mei 2023.

World Economic Forum (2022) “Scientists Count the World’s Tree Species’ (Spoiler: it’s a Bunch). Inapatikana katika https://www.weforum.org. Ilisomwa tarehe 10 Mei 2023.